## USIWAOGOPE MANABII, WAPIME

Dhambi ilikata mawasiliano kati ya Mungu na mwanadamu, lakini kwa upendo wake Mungu alitafuta njia nyingine ya mawasiliano. "Kisha akawaambia, Sikilizeni basi maneno yangu; akiwapo nabii kati yenu, Mimi, BWANA, nitajifunua kwake katika maono, nitasema naye katika ndoto" (Hes.12:6). Nabii akiwa katika maono macho yake yanatazama na kuona mambo ambayo Mungu anamwonesha; watu wengine walio karibu naye hawawezi kuona mambo hayo; waweza kusikia sauti au tetemeko (Dan.10:7; Mdo.9:3-7). Ndoto huja usiku anapolala; anaoneshwa mambo fulani muhimu anayopaswa kuwaambia watu wa Mungu au kuwaonya mataifa. Wakati mwingine Mungu anamtuma malaika wake na ujumbe maalumu kwa nabii (Dan.9:20-23; Ufu.19:9,10)

Mungu hawezi kuliangamiza taifa lo lote bila kuwasiliana na manabii wake ile watoe onyo mapema kusudi watu wale wajirekebishe nyendo zao. "Hakika Bwana Mungu hatafanya neon lo lote bilz kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake" (Amosi 3:7). Nuhu, Ibrahimu na Yona walipewa ujumbe maalumu wa maangamizi ya wanadamu na walitoa onyo. Waliojirekebisha hawakuangamizwa; wale waliokataa kujirekebisha waliangamizwa (Yer.18:7-10; Mwanzo Sura ya 18 na 19; Yuda 7; 2 Pet.2:6; Yona 3 hadi 4:1). Dunia hii ya sasa inafanana na Sodoma na Gomora na manabii wanatupasha habari kuwa itateketezwa kwa moto kama Sodoma na Gomora (2 Pet.3:1-7,10).

Kwa kuwa sisi ni watu wa kawaida, hatujui Mungu anakusudia kufanya nini hapa duniani, ni jambo la muhimu mno kuwasikiliza manabii wake. "Angalieni msimkatae yeye anenaye. Maana ikiwa hawakuokoka wale waliomkataa yeye aliyewaonya juu ya nchi, zaidi sana hatutaokoka sisi tukijiepusha na yeye atuonyaye kutoka mbinguni" (Ebr.12:25,26). Mungu ndiye anayewapasha habari za matukio duniani manabii wake. Hivyo tutapata hasara sisi wenyewe tukiwapuuzia, wala hatutafanikiwa katika safari yetu ya mbinguni. "…mwaminini BWANA, Mungu wenu, ndivyo mtakavyothibitika; ***waaminini manabii wake***, ***ndivyo mtakavyofanikiwa***" (2 Nya.20:20).

Haitoshi kujihami na kusema kila nabii anayekuja ni nabii wa uongo maana manabii wa kweli wapo pia hadi mwisho wa dunia (1 Kor.12:28; Efe.4:8,11-14). Je, kanisa limefikia umoja wa imani sasa? Hapana. Je, kanisa limefikia cheo cha kuwa na tabia kama ile ya Yesu? Hapana. Je, waumini wanamfahamu sana Yesu? Hapana. Kwa ajili hiyo tunawahitaji manabii na wahudumu wengine kutoa huduma yao ndani ya kanisa la Mungu.

Unabii wa Yoeli 2:28-32 ulitimia kwa sehemu tu siku ile ya Pentekoste (Mdo.2:17-21). Kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste ni "mvua ya vuli." Tunangojea "mvua ya masika" Roho Mtakatifu atakapomwagwa tena itakapotangazwa Amri ya Jumapili kwa ulimwengu mzima na kulazimishwa (Ufu.13:16,17; 18:1-4). Uwezo wa Roho Mtakatifu utakuwa mara kumi kuliko ule wa Pentekoste na watu wa Mungu waliodanganywa watarudi katika zizi la Kristo (Ufu.18:4; Yn.10:16).

Ni kweli Yesu alionya, akisema, "Jihadharini na manabii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa-mwitu wakali. Mtawatambua kwa matunda yao" (Mt.7:15,16). Wamo ndani ya makanisa, wanatumia jina la Yesu, lakini wametumwa na Shetani kuwadanganya wateule ili wapotee na kujitenga mbali na Mungu (1 Kor.11:13-15; Yer.14:14:16; Mt.24:11,24; 7:15-23). Habari njema ni kwamba tutawatambua. Viko vipimo vikuu vinne vya kuwapima manabii kama wametumwa na Mungu au na Shetani. Lazima nabii atimize vyote vinne, akishindwa kimoja hafai.

***Kipimo cha Kwanza: Sheria na Ushuhuda (Isa.8:20).*** Wapimwe kwa Amri Kumi za Mungu, pia mafundisho yao yapimwe kwa Biblia. "Na waende kwa Sheria na Ushuhuda; ikiwa hawasemi

sawasawa na neon hili, bila shaka kwa hao hapana asubuhi" (Isa.8:20). Wakivunja moja tu wamevunja zote (Yak.2:10-12). Karibu zaidi ya asilimia tisini na tano ya manabii watatupwa mbali kwa kipimo hiki peke yake; hata mtu asiyeijua Biblia anaweza kuwapima bila shida. Kwa vile Amri za Mungu zimebadilishwa, hapa nanukuu kama zilivyotangazwa mlimani Sinai:

**I. Usiwe na miungu mingine ila Mimi.**

**II. Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.**

**III. Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.**

**IV. Ikumbuke siku ya sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako. Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya sabato akaitakasa.**

**V. Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.**

**VI. Usiue.**

**VII. Usizini.**

**VIII. Usiibe.**

**1X. Usimshuhudie jirani yako uongo.**

**X. Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako.**

Manabii wengi wanaojitapa watatupwa nje kwa kipimo hiki kimoja.

***Kipimo cha Pili: Matunda au Maisha yao (Mt.7:20).*** "Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua" (Mt.7:20). Hiki si rahisi mpaka uwe umekaa na nabii huyo kwa kipindi fulani na kujua tabia yake. Lakini yaliyo moyoni mwa mtu mara nyingi yanatoka kinywani mwake na kudokeza tabia yake. Pia mafundisho yake yapimwe kama yanawafanya watu wamjue Yesu zaidi au yanawapeleka mbali naye.

***Kipimo cha Tatu: Kukubali kuwa Yesu alikuwa na mwili kama wetu (1 Yoh.4:1-3).*** "Wapenzi, msiiamini kila roho, bali zijaribuni hizo roho, kwamba zimetokana na Mungu; kwa sababu *manabii wa uongo wengi wametokea duniani.* Katika hili mwamjua Roho wa Mungu; kila roho ikiriyo kwamba Yesu Kristo amekuja katika mwili yatokana na Mungu. Na kila roho isiyomkiri Yesu haitokani na Mungu. Na hii ndiyo roho ya Mpinga Kisto ambayo mmesikia kwamba yaja..." (1 Yoh.4:1-3). Yesu asingetusaidia kitu kama angekuwa na mwili tofauti na wetu, maana angetumia nguvu za Mungu kushinda majaribu. Habari njema ni kwamba alikuwa na mwili kama wetu, hivyo anaweza kutusaidia (Ebr.2:14-18; 4:14-16; Yn.1:1-3,10,14).

***Kipimo cha Nne: Unabii Uliotimia (Yer.28:9).*** "Nabii atabiriye habari za amani, neno la nabii yule litakapotokea, ndipo nabii yule atakapojulikana, kuwa BWANA amemtuma kweli kweli" (Yer.28:9). Lakini tahadhari kubwa! "Kukizuka katikati yako nabii, au mwotaji wa ndoto, akikutolea ishara au ajabu, ikatukia hiyo ishara au hiyo ajabu aliyokuambia, akisema, Na tuifuate miungu mingine usiyoijua, tuitumikie hiyo; wewe usiyasikize maneno ya nabii yule, au yule mwotaji wa ndoto; kwa kuwa BWANA, Mungu wenu, yuawajaribu, apate kujua kwamba mwampenda BWANA, Mungu wenu, kwa mioyo yenu yote na roho zenu zote…" (Kum.13:1-11).

Usiwaogope manabii au mitume, wapime kwa vipimo hivyo vinne, utawatambua walio wa kweli na wa uongo.

Mfululizo na.15#mm

[TOA FOTOKOPI, UMGAWIE MWENZAKO]

.